

MWALIKO WA KUPOKEA MAONI NA MAHITAJI YA MFUMO WA KIELETRONIKI WA KUFANYA USAILI WA KUANDIKA (ONLINE APTITUDE TEST SYSTEM)

Ofisi ya Rais-Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imekuwa ikipokea maoni mbalimbali kutoka kwa wadau wetu juu ya namna ya kuboresha mchakato wa ajira. Mathalan, katika kipindi cha Mwaka 2010-2014, wadau wetu mlitoa maoni ya namna bora ya kupokea maombi ya kazi na hivyo kupelekea kuanzishwa kwa mfumo wa kupokea na kuchakata maombi ya kazi unaojulikana kwa jina la **Ajira Portal**.

Licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa Ajira Portal, Sekretarieti ya Ajira imepokea maoni na changamoto mbalimbali kutoka kwa wadau wetu wa namna ya tunavyoendesha usaili wa kuandika kwa sasa. Kutokana na maoni hayo, Sekretarieti ya Ajira imeanza kuendesha saili za kuandika kwenye kanda mbalimbali ili kuwapunguzia gharama na usumbufu wadau wetu hususan waombaji fursa za ajira.

Hata hivyo, ili kupata suluhisho la kudumu, Sekretarieti ya Ajira imeanza mchakato wa kujenga mfumo wa kieletroniki ambao utawawezesha waombaji wa fursa za ajira kufanya usaili wa kuandika kwenye ngazi za Mkoa na Wilaya kupitia vituo maalum.

Ili kufanikisha zoezi hilo, Sekretarieti ya Ajira inatarajia kukusanya maoni na mahitaji ya mfumo huu kutoka kwa wadau wake na **hususan waombaji kazi** katika vituo vya Dodoma na Dar es Salaam katika kumbi ambazo mtajulishwa. Vikao hivi vya wadau vitafanyika kuanzia tarehe 09 -12 Januari 2023. Kwa kituo cha Dodoma, kikao cha wadau kitafanyika tarehe 9 Januari, 2022 na Dar es Salaam kitafanyika tarehe 11-12 Januari, 2022.

Kupitia tangazo hili, wadau wetu wote mliopo ndani ya Mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam mnaalikwa kushiriki katika kutoa maoni yenu kwa kutuma majina matatu, jinsia, ngazi ya elimu, utaalamu wa fani uliyosomea, namba ya simu pamoja na Mkoa ulipo kupitia barua pepe ya mfumo@ajira.go.tz kabla au ifikapo tarehe **07 Januari 2023 saa**

sita (06:00) mchana. Baada ya hapo kamati yetu iliyopangwa kupokea maoni ya wadau hao itachambua na kuchagua wadau 100 kwa kuzingatia Jinsi, uwakilishi wa kada kwa kila taaluma, ngazi za elimu pamoja uwakilishi wa Makundi maalum kushiriki katika zoezi hili.

Aidha, kwa wadau wetu mlioko nje ya Mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam na mngenda kutoa maoni yenu, mnaalikwa kutuma maoni yenu kwa kutumia barua pepe maoni@ajira.go.tz kabla ya tarehe **12 Januari 2023**.